

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU**

18 APRILI, 2019



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 18 APRILI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**107. MHESHIMIWA SUZANA CHOGISASI MGONUKULIMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Watu wenye Ulemavu wa Macho wanakosa haki ya kuchagua Viongozi wanaowataka kutokana na kusaidiwa kupiga kura na watu wengine ambao wanaweza kuwapigia kura kinyume na ridhaa

zao, hivyo kura zao kwenda kwa watu ambao si chaguo lao:-

Je, Serikali iko tayari kuchapisha karatasi maalum za kupiga kura kwa kutumia mfumo wa Nukta Nundu kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu wa Macho.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**108. MHESHIMIWA DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF (MGOGONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Zanzibar kwa namna ilivyo inahitaji uchumi wa Visiwa ambapo Bandari ni kitu cha lazima:-

Je, Serikali ya Muungano inaungaje mkono nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga Bandari kubwa.

**109. MHESHIMIWA MARTHA MOSES MLATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-



Je, ni kwa nini Sherehe za Muungano zimekuwa zikifanyika na kupewa nafasi kubwa Kitaifa tu.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**110. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSEKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wananchi wa Busekelo katika Kata ya Luteba walianza kutengeneza barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe kupitia Milima ya safu za Livingstone:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kuunga mkono juhudi za Wananchi hao.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**111. MHESHIMIWA EDWARD FRANZ MWALONGO (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahudumia Wagonjwa wa Akili wanaozurura mitaani katika masuala ya matibabu, mavazi na makazi.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
18 APRILI, 2019**



**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**

**BUNGE LA TANZANIA**